**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

SHULE YA SEKONDARI IFUMBO,

S L P 47,

CHUNYA.

06/12/2021

KUMB. NA.IF/C/UT.J/VOL.I /14/21

JINA LA MWANAFUNZI.....................................

S L P 139,

CHUNYA.

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IFUMBO MWAKA WA MASOMO 2021.**

Uongozi wa shule ya sekondari Ifumbo unayofuraha kubwa sana kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ifumbo. Shule ipo katika kata ya Ifumbo wilayani chunya. Ipo umbali wa kilomita arobaini na nne (44 km) kusini magharibi mwa makao makuu ya wilaya.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 hivyo unatakiwa kufika shuleni bila kukosa wala kuchelewa tarehe hiyo saa 01:30 asubuhi ukiwa na mzazi/mlezi wako. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 Baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi/mlezi ambaye mtoto wake hataripoti shuleni.

Nafasi uliyopewa ni bahati sana, wapo wengi wangependa kupata lakini wameikosa hivyo unatakiwa uitumie vizuri kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

Aidha unatakiwa kuzingatia kuwa wakati wote ukiwa mwanafunzi katika shule hii kigezo cha upimaji maendeleo yako itakuwa :- NIDHAMU BORA, TAALUMA BORA na UTENDAJI WA KAZI ZA NJE. Ukiwa shuleni na nje ya shule.

Pamoja na barua hii pokea, viambatanisho vifuatavyo:-

1. Sheria na kanuni za shule ambazo unatakiwa uzisome kwa makini na kuzielewa kisha uzifuate muda Wote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii ndani na nje ya shule.
2. Orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima uje navyo shuleni.
3. .Fomu ya uthibitisho wa uraia wako, ikiwa una cheti cha kuzaliwa leta nakala yake.
4. Fomu ya uthibitisho wa afya yako.
5. Fomu ya mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelezo mengine yatakayotolewa na

Unatakiwa kuzikamilisha fomu hizi na kuzileta pamoja na barua hii ufikapo shuleni.

***KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IFUMBO***

..........................................

**CHRISPIAN M KAZIMILI** THE HEADMASTER IFUMBO SEC. SCHOOL

**MKUU WA SHULE**

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

## SHULE YA SEKONDARI IFUMBO

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

***MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA/ KUFUKUZWA SHULE***

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

Aidha uongozi wa shule hauta mfumbia macho mwafunzi yeyote atakaye kiuka sheria na kanuni zashule.

***IMETOLEWA NA MKUU WA SHULE***

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

***SARE ZA SHULE***

**WAVULANA**

i. Suruali mbili (2) rangi ya kijani na kaki tetroni zivaliwe na
ii. Mkanda mweusi saizi ya kawaida
iii. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi (tetroni)
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili (2) visiwe na visigino virefu.
v. Soksi nyeusi Zaidi ya jozi mbili.
**vi.** Sweta mbili (2) rangi ya kijani na kaki.
vii. Nguo za michezo mwanafunzi atazitumia wakati wa mazoezi (tracksuit ya blue na T-shirt ya shule.)

**WASICHANA**

i. Sketi mbili za malinda rangi ya kijani na kaki tetroni.
**ii. Mashati mawili meupe yenye kora mikono mifupi (Tetroni)**
iii. Viatu vya ngozi vyenye kamba jozi mbili visiwe na kisigino kirefu.
iv. Soksi nyeupe Zaidi ya jozi mbili
v. Sweta mbili (2) rangi ya kijani na kaki.
vi. Nguo za michezo mwanafunzi atazitumia wakati wa mazoezi (tracksuit ya blue na T-shirt yas hule)
vii. Hijaburanginyeupe (waislam).

**NB**:-*Ili kuepukamchanganyiko wa rangi na aina ya kitambaa sketi kwa wasichana na suruali kwa Wavulana zitashonwa kwa fundi mmoja tu kwa gharama ya Tsh……………kwa suruali/sketi.*

NB: AJE NA DAFTARI KUMI (10) QUIRE 3 4 2, MKEBE NA KALAMU ZA KUANDIKIA.

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

SHULE YA SEKONDARI IFUMBO

## FOMU YA KUKUBALI

1. Mimi ........................................................nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ifumbo kama mwanafunzi wa kutwa tarehe .................... nitafika shule bila kuchelewa .
2. Nitatii sheria na kanuni za shule, sitajihusisha wala kuchochea migomo shuleni nitakuwa mwanafunzi mwaminifu na mwenye bidii katikama somo na kazi za kujitegemea.
3. Sahih iya mwanafunzi.........................

## SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi ......................................... nimekubali mtoto wangu ................................................ Asome katika shule ya sekondari Ifumbo kuanzia tarehe................................................
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shule ni kama ilivyotajwa katika barua.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea .
4. Ninakubali mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya sekondari Ifumbo kama mwanafunz iwa kutwa na ataendelea hivyo hadi atakapomaliza kidato cha nne (iv) . Hivyo mimi pamoja na mwanangu hatutamsumbua mkuu wa shule kwa vyovyote kuhusu mipango ya malazi au uhamisho kwenda shule za bweni.
5. Anwani yangu ya kudumu

   ......................................................
   ......................................................
   ......................................................
   ......................................................

Sahihi ...............................................

Tarehe...............................................

Namba ya simu...............................

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MKOA...............**

**OFISI YA MKUU WA WILAYA** **WILAYA.............**

**S L P............**

**TAREHE.........................**

**KUMB NA..............................**

**MKUU WA SHULE,**

**SHULE YA SEKONDARI IFUMBO,**

**S L P 47,**

**CHUNYA.**

**YAH:UTHIBITISHO WA URAIAWA TANZANIA.**

Nathibitisha kuwa ...........................................................(jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa / kuandikishwa.

Baba yake (jina kamili)...........................................amezaliwa katika mkoa wa .............. wilaya............... tarafa ya................ kata ya.............

Mama yake (jina kamili) .....................................amezaliwa katika mkoa wa ...................................

Wilaya ya................. tarafa ya ........................... Kata ya........................hapa nchini.

...........................................

**MKUU WA WILAYA**

**NB**: Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu ikijazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule tarehe ya kuripoti shuleni

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

**CHUNYA DISTRICT COUNCIL**

**IFUMBO SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL FORM

**PART A.**

Mr/miss.......................................................

Please, examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school.

Thank you.

**PART B.**

**CATEGORIES OF EXAMINATION**

1. P.V bleeding...........................................................
2. Hemoglobin........................................................
3. Sight...................................................................
4. Blood pressure.................................................
5. Urine for sugar............................................................
6. Pregnancy test.............................................................
7. Stool for routine examination...........................................
8. Asthma.........................................................................
9. Skin disease.............................................................
10. Leprosy...................................................................
11. Any deformity.........................................................
12. Epilepsy..................................................................
13. Pulmonary tuberculosis..................................................
14. Neurosis...................................................................
15. Venereal disease ........................................................
16. Other serious disease ......................................................

**PART C.**

**MEDICAL CERTIFICATION**

I have examined the above named student and consider that he/she is physically and mental fit / physically and mentally unfit for a fulltime.

Thank you.